# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# SERA YA MAENDELEO YA USHIRIKA, 1997

## WIZARA YA KILIMO NA USHIRIKA

*DAR ES SALAAM* *JANUARY 1997*

# SERA YA MAENDELEO YA USHIRIKA, 1997

## YALIYOMO


| | | |
|---|---|---|
| UFAFANUZI | | (i) |
| 1.0 | UTANGULIZI | 1 |
| 1.1 | USULI | 1 |
| 1.2 | UHALALI WA SERA | 3 |
| 2.0 | MALENGO YA SERA YA MAENDELEO YA USHIRIKA | 4 |
| 3.0 | KAULI ZA SERA | 5 |
| 4.0 | MIKAKATI YA UTEKELEZAJI | 7 |
| 4.1 | Mikakati ya Jumla | 7 |
| 4.2 | Mikakati ya Ushirika wa Mauzo ya Mazao ya Kilimo | 9 |
| 4.3 | Mikakati ya Huduma za Fedha Vijijini | 10 |
| 4.4 | Mikakati ya Ushirika wa Wafugaji | 12 |
| 4.5 | Mikakati ya Ushirika wa ujenzi wa Nyumba | 13 |
| 4.6 | Mikakati ya Ushirika wa Viwanda | 13 |
| 4.7 | Mikakati kwa Aina Nyingine za Ushirika | 13 |
| 5.0 | USIMAMIZI NA UHAKIKI WA SERA | 14 |
| 6.0 | HITIMISHO | 14 |

## UFAFANUZI

### Chama cha Ushirika ni Kitu Gani?

(Tafsiri kutoka Pendekezo la ILO la 172 la 1996)

Chama cha ushirika ni muungano wa watu ambao kwa hiari yao wanaungana na kufanikisha lengo la pamoja kwa kuanzisha chombo kinachoendeshwa kwa misingi ya kidemokrasia, kwa kuchangia kwa uwiano mtaji unaotakiwa na kugawana kwa haki ziada inayotokana na biashara ya chama ambacho wanachama hushiriki kwa makini.

## 1.0 UTANGULIZI

### 1.1 USULI

Mwaka 1995 Shirikisho la Ushirika Duniani (ICA) lilisheherekea miaka 100 tangu kuanzishwa kwake. Vilevile mwaka 1995 ulikuwa ni mwaka wa mia moja na hamsini tangu chama cha kisasa cha kwanza kilipoanzishwa na waasisi wa ushirika huko Rochdale nchini Uingereza. Kukua na kuenea kwa ushirika kulisababishwa na mabadiliko makubwa ya kiuchumi, kijamii, na kisiasa yaliyotokea Ulaya mwishoni mwa karne ya 18 hadi karne yote ya 19 na hasa mapinduzi ya viwanda na kutoweka kwa mfumo wa ukabaila na kuzaliwa kwa ubepari.

**Mfumo wa zamani ulivunjika**

Ubepari ulisababisha kuanza kwa mfumo wa maisha ya mijini, mfumo ambao ulisababisha hali ngumu ya maisha kwa tabaka la wafanyakazi. Sehemu za vijijini pia zilikabiliwa na hali ngumu ya maisha, wakulima walidaiwa madeni makubwa na wakopeshaji wa fedha. Matokeo ya vurugu, ukosefu wa amani na utulivu katika jamii yalijenga haja ya mtazamo mpya kiuchumi na kijamii.

Kuanzia wakati huo, changamoto na lengo la ushirika imekuwa ni kurekebisha mfumo wa kijamii na kiuchumi ili kuboresha maisha duniani yenye sifa za kidemokrasia, haki, usawa na kujitegemea.

Nchini Tanzania ushirika ulianza mwaka 1925 kwa kuandikisha chama kilichoitwa Chama cha Wakulima Wananchi wa Kilimanjaro (Kilimanjaro Native Planters Association (KNPA))

Wakulima wadogo wadogo walijiunga pamoja na kuanzisha ushirika ili kujikomboa kijamii na kiuchumi kutoka kwenye makucha ya wafanyabiashara wa Kizungu na Kiasia. Inakadiriwa kuwa wakulima hawakulipwa kiasi cha asilimia 40 ya pamba yao iliyokuwa inanunuliwa na wafanyabiashara wa Kiasia katika miaka ya 1930 na 1940.

Kabla ya uhuru wanachama wenyewe ndio waliokuwa wakianzisha na kuendesha ushirika wao. Kazi ya serikali ilikuwa ni kutoa habari, uhamasishaji, elimu, mafunzo, ukaguzi na usimamizi. Ushirika ulikuwa huru na ulizingatia kanuni ya kujitegemea. Ushirika wa leo umerithi mali nyingi za ushirika huu wa kabla ya uhuru kama vile majengo, mitambo, n.k.

Baada ya uhuru, kutokana na mafanikio ya ushirika katika sehemu chache nchini, serikali ilichukua jukumu la kuanzisha na kuendesha ushirika. Kwa makusudi serikali ilisimamia uanzishaji wa ushirika. Ushirika ulijumuishwa moja kwa moja kwenye malengo ya kitaifa badala ya kufuata matakwa na malengo ya wanachama wa ushirika. Hii ilichangia kwa kiasi kikubwa kukosekana kwa mitaji kutoka ndani ya ushirika na hivyo ushirika kuwa tegemezi kwa serikali na kuendeshwa kwa mikopo.

Zaidi ya hayo maendeleo ya rasilimali yaliyotokana na watu pamoja na uwezo wa majenzi ambao ulihudumiwa na ushirika wenyewe ulikufa na kuangukia mikononi mwa serikali. Kuanzia katikati ya miaka ya 1970 ushirika ulikuwa moja kwa moja chini ya miliki na udhibiti wa serikali na hivyo kukosa

sifa za ushirika za kimataifa. Kutokana na uwezo mdogo wa Serikali kirasilimali ushirika uligeuka kuwa mzigo mkubwa kwa serikali yenyewe na kwa uchumi wa taifa kwa ujumla.

Pamoja na yote hayo, ushirika katika aina zake mbali mbali ni mhimili muhimu katika maendeleo ya kijamii na kiuchumi kwa nchi yoyote ile. Ushirika huyashirikisha makundi yote ya jamii katika maendeleo kama vile wanawake, vijana, wazee na walemavu.

Kwa vile serikali inatambua nafasi na mchango wa ushirika katika kutatua matatizo ya kiuchumi, kijamii na mazingira, basi itaheshimu na kufuata kanuni za ushirika kama zilivyoainishwa na Muungano wa Kimataifa wa Vyama vya Ushirika (ICA) ambazo ni:-

- Uanachama wa hiari na wazi;
- Uongozi wa kidemokrasia;
- Ushiriki wa wanachama katika shughuli za kiuchumi;
- Kujitawala na kujitegemea;
- Elimu, mafunzo na habari;
- Ushirikiano baina ya vyama vya ushirika;
- Kuijali jumuiya;

## 1.2 UHALALI WA SERA

Kukosekana kwa sera rasmi ya ushirika kumesababisha mabadiliko ya mara kwa mara katika sekta ya ushirika kimuundo na kimtazamo, kama vile kijiji kupewa hadhi ya chama cha ushirika na wanakijiji kupewa uanachama kwa mujibu wa sheria kinyume na kanuni za ushirika.

Kuwepo kwa sera ya maendeleo ya ushirika ikianisha madhumuni, malengo na mikakati kutapunguza kwa kiasi kikubwa ukiukwaji wa misingi ya ushirika ya kimataifa iliyowekwa na ICA na hivyo kuwezesha matumizi ya kanuni za ushirika ili kuleta maendeleo ya kijamii na kiuchumi kwa walio wengi.

## 2.0 MALENGO YA SERA YA MAENDELEO YA USHIRIKA

Tofauti na wafanyabiashara wenye ujuzi na uzoefu katika uzalishaji na uendeshaji wa shughuli za kibiashara, ushirika unalenga watu wasio na ujuzi wala uzoefu wa shughuli za kibiashara. Ushirika huundwa na makundi yenye uwezo mdogo wa kupata rasilimali za kuzalishia kama vile wakulima wadogo wadogo, watu wasio na ardhi, wanawake, vijana, wazee na walemavu. Ni nia ya serikali kuona kuwa wananchi wake wote wanajihusisha na shughuli za uzalishaji ili kujiongezea kipato.

Kwa hiyo madhumuni ya sera ya maendeleo ya ushirika ni:-

2.1 Kubainisha ukweli kuwa ushirika ni chombo muhimu kwa maendeleo ya jamii, uchumi na utamaduni pamoja na maendeleo ya wananchi kwa ujumla.

2.2 Kuutambua mchango wa ushirika katika misingi ya uongozi wa kidemokrasia katika shughuli za kiuchumi haki na usawa katika kugawana ziada.

2.3 Kufuata na kuheshimu itikadi ya ushirika na kuitekeleza ili kuhakikisha ushirika unakuwa huru.

2.4 Kuweka mazingira mazuri yatakayowawezesha watu kujumuika pamoja na kutumia rasilimali zao kwa maendeleo yao ya kiuchumi na kijamii.

2.5 Kusaidia maendeleo ya ushirika hasa katika elimu, mafunzo na kujenga uwezo wa kitaasisi.

## 3.0 KAULI ZA SERA

3.1 Serikali inaunga mkono, inaafiki na kuthamini dira ya ushirika ya kuleta haki na usawa wa kijamii na kiuchumi katika jamii.

3.2 Serikali inaheshimu na kulinda uhuru wa ushirika wa kujiendesha, hata hivyo serikali haitasita kuvifuta vyama vya ushirika ambavyo vitakiuka misingi na kanuni za ushirika.

3.3 Serikali inatambua aina mbalimbali za ushirika kama vile:-

- Ushirika wa kilimo wa uzalishaji na usindikaji;
- Ushirika wa ugavi vijijini;
- Ushirika wa kuendeleza ardhi;
- Ushirika wa walaji;
- Ushirika wa uvuvi;
- Ushirika wa huduma;
- Ushirika wa wasanii;

- Ushirika wa wafanyakazi wa uzalishaji;
- Ushirika wa akiba na mikopo;
- Benki za ushirika;
- Ushirika wa ujenzi wa nyumba;
- Ushirika wa usafirishaji;
- Ushirika wa bima;
- Ushirika wa afya;

3.4 Serikali itaboresha sheria ili kuulinda ushirika.

3.5 Serikali itachochea maendeleo ya ushirika kwa kuboresha upatikanaji wa habari, uhamasishaji, elimu, mafunzo ukaguzi na usimamizi.

3.6 Serikali itawahamasisha wanawake kushiriki kwenye ushirika kwa kuondoa sheria, utamaduni, mila na vikwazo vingine vinavyowazuia wanawake kushiriki kwenye ushirika.

3.7 Serikali kama itakavyoonekana inafaa, itaviandikisha, kuvifuta au kuvifilisi vyama vya ushirika.

3.8 Serikali itaanzisha elimu ya ushirika shuleni na vyuoni ili kuwaandaa vijana waweze kujiajiri na kujitegemea.

3.9 Serikali itatilia mkazo utafiti katika nyanja mbali mbali zinazoathiri shughuli za ushirika kama vile ubora wa bidhaa, uzalishaji, uwekezaji wa vitega uchumi, n.k.

3.10 Serikali itadumisha uhusiano mzuri na wahisani mbali mbali na serikali zingine. Mkazo mkubwa utakuwa kwenye elimu, mafunzo na katika kujenga uwezo wa kitaasisi.

3.11 Serikali itasaidia pale inapowezekana kwenye maendeleo ya watu, na katika kujenga uwezo wa ushirika.

3.12 Serikali itauhamasisha ushirika ili uondokane na dhana ya biashara pekee na hivyo kujumuisha uzalishaji, usindikaji na mauzo ili kupata faida zaidi na hivyo kuongeza pato la wanachama wake.

3.13 Serikali inaunga mkono ushirika katika juhudi zake za kuhifadhi mazingira.

## 4.0. MIKAKATI YA UTEKELEZAJI

### 4.1. Mikakati ya Jumla

Mazingira ya sasa ya kijamii, kiuchumi na kisiasa ni mazuri kwa maendeleo ya ushirika. Mafanikio ya ushirika yanategemea mambo mengi ikiwa ni pamoja na kuongezeka kwa wanachama, ufanisi, uwazi na uwajibikaji wa viongozi wake kwa wanachama na ushirikishwaji wa wanachama katika uendeshaji wa vyama vya ushirika.

Mikakati ifuatayo ya jumla itatumika:-

4.1.1. Kuwapa wanachama madaraka kwa njia ya elimu na mafunzo mara kwa mara.

4.1.2. Kupendekeza vyama vya msingi kuungana kwa lengo la kuongeza uwezo wao kiuchumi kulinganisha na vyama vikuu.

4.1.3. Kuendeleza miundo ya mgatuo wa ushirikishwaji ambao utaimarisha upatikanaji wa taarifa na uwazi kwa wanachama.

4.1.4. Kuboresha sheria ya ushirika itakayoweka misingi ya uwajibikaji wa uongozi wa ushirika kwa wanachama na adhabu kali punde sheria zikikiukwa.

4.1.5. Kuimarisha ukaguzi na usimamizi wa vyama vya ushirika ili kuzuia mapema vitendo vya ufujaji mali za chama.

4.1.6. Kuanzisha taratibu zitakazoilazimu sekta ya ushirika kuchangia gharama za elimu, mafunzo, ukaguzi na usimamizi.

4.1.7. Kuboresha mazingira ya kazi ya watumishi wa vyama vya ushirika ili kuwavutia na kuwatunza watumishi bora katika ushirika.

4.1.8. Kutumia kwa ukamilifu msingi wa kujitegemea kwa kuongeza hisa, kuanzisha mifuko maalum na taasisi za fedha za ushirika.

## 4.2. Mikakati ya Vyama vya Ushirika vya Mazao

Vyama vya ushirika vya mazao vinapaswa kukua na kuwa vituo vya ugavi na uenezi wa pembejeo za zana za kilimo, teknolojia na mafunzo. Hali hii itawawezesha wakulima kuwa na sauti dhidi ya washindani wao na kushiriki katika soko, ili kuongeza kipato chao na maisha bora.

Lengo hili litafikiwa kwa hatua zifuatazo:-

4.2.1. Kumhamisha mkulima toka kilimo cha kujikimu na kumwingiza katika kilimo cha kibiashara kwa kutumia misingi ya kilimo bora na takwimu za masoko.

4.2.2. Kuwawezesha wakulima kuwa wachambuzi makini wa matatizo yao, kuelewa njia mbali mbali za kujiimarisha kiuchumi, gharama za uzalishaji na bei za mazao katika soko, ili kuwawezesha kutumia rasilimali kwa ufanisi kwa ajili ya kuzalisha mazao ya kilimo na mifugo yenye kuvutia bei nzuri.

4.2.3. Kutoa elimu ya mazingira na matumizi ya kuendeleza rasilimali ili kuzuia kilimo kinachopelekea mmomonyoko wa ardhi, ongezeko la asidi ardhini, ukataji miti ovyo na uharibifu wa mazingira kwa ujumla.

4.2.4. Kuingiza taratibu za uwazi wa uwajibikaji katika ushirika.

4.2.5. Kuongeza pato la mkulima kwa kuongeza thamani ya mazao kwa kusindika, na matumizi ya mbegu bora.

4.2.6. Kuwapa elimu wataalam wa huduma ya ushauri ili kwa ushirikiano na maafisa ushirika watoe mafunzo ya uwiano kamili kwa wakulima.

4.2.7. Kuorodhesha shughuli zisizo za kilimo ili kuwapatia wakulima mapato wakati wa kiangazi.

4.2.8. Kuanzisha taasisi za fedha sambamba na chama cha ushirika wa mazao ili kukusanya amana na kutoa mikopo kwa wakulima na chama kwa ajili ya ununuzi wa mazao.

## 4.3 Mikakati ya Huduma za Fedha Vijijini

Kwa muda mrefu sehemu kubwa ya shughuli za vyama vya ushirika hutegemea mikopo. Tangu miaka ya 70 hapakuwepo na uwekaji wa akiba, uanzishaji wa mifuko maalum, uongezaji hisa wala uanzishaji wa benki, vitu ambavyo ndiyo misingi ya kujitegemea. Kwa hiyo Vyama vya ushirika vitahimizwa kutumia misingi ya kujitegemea.

Katika kipindi cha miaka saba (7) kutokana na mikakati thabiti, ushirika utaweza kujitegemea kwa kiasi kikubwa kifedha kwa matumizi ya muda mfupi na hivyo kulinda uhuru wake, kuongeza uzalishaji na mapato kwa wanachama.

Malengo hayo yatafikiwa kwa mbinu zifuatazo:-

4.3.1. Kuongeza idadi ya wanachama kwa njia ya elimu na mafunzo.

4.3.2. Kubuni vivutio mbali mbali ili wanachama waongeze hisa.

4.3.3. Kuhimiza uanzishaji wa mifuko maalum kwa shughuli mbalimbali kama vile upatikanaji wa pembejeo na ukusanyaji wa mazao.

4.3.4. Uhamasishaji wa uanzishaji wa vyama vya akiba na mikopo ambavyo vitatoa huduma za kifedha uwekezaji amana, riba na mikopo.

4.3.5. Uhamasishaji wa uanzishaji wa benki za ushirika katika ngazi za wilaya/mikoa.

4.3.6. Kipaumbele kitatolewa katika kuimarisha taasisi za huduma za fedha vijijini kwa njia ya elimu na mafunzo.

4.3.7. Serikali itaimarisha idara ya ushirika ili kutoa elimu na mafunzo.

4.3.8. Serikali itaimarisha huduma ya ukaguzi na usimamizi wa taasisi za fedha vijijini.

4.3.9. Walengwa wa maendeleo ya ushirika ni wanachama. Madaraka ya wanachama kupitia taarifa za mara kwa mara, taarifa za uendeshaji na taarifa za ukaguzi, yatalindwa kisheria.

## 4.4 Mikakati ya Ushirika wa Wafugaji

Tanzania inayo rasilimali kubwa ya kuendelezea sekta ya mifugo kwani ina zaidi ya hekta milioni 60 za malisho yenye uwezo wa kufuga ng'ombe milioni 20. Lakini sekta hii haijaendelezwa na hivyo kushindwa kudumisha mapato na maisha ya wafuagaji wenyewe na uchumi wa taifa kwa ujumla. Mipango ya kuendeleza ushirika wa mifugo ni:-

4.4.1. Kwa ushirikiano na idara ya mifugo, idara ya ushirika itafanya utafiti kuelewa mazingira halisi, taratibu za masoko, nafasi ya ushirika na vikwazo katika kuendeleza sekta hii.

4.4.2. Kuhamasisha ushirika wa wafugaji kwa pamoja na wataalam wa mifugo.

4.4.3. Kuelimisha wanachama juu ya umuhimu wa kuongeza hisa, kuanzisha mifuko maalum kwa ajili ya upatikanaji wa madawa, vifaa, chakula cha mifugo, matengenezo ya majosho na uwekezaji mwingine.

4.4.4. Kuanzisha programu za mafunzo yanayofaa kwa ajili ya wafanyakazi wa ushirika wa masoko kwa kuandika upya kitabu cha kiongozi kwa ajili ya mameneja wa vyama vya mauzo ya mifungo.

4.4.5. Kuendeleza na kukarabati vifaa vya soko la ndani la mifugo nchini Tanzania.

## 4.5 Mikakati ya Ushirika wa Ujenzi wa Nyumba

Wizara ya Maendeleo ya Ardhi na Miji itaendelea kutoa utaalam wa ujenzi kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo na Ushirika.

## 4.6 Mikakati ya Ushirika wa Viwanda

Inategemewa kuwa Ofisi ya Makamu wa Rais (kufuta umaskini), Wizara ya Viwanda na Biashara (SIDO na SICATA), Wizara ya Kazi na Vijana, Wizara ya Nishati na Madini zitaendelea kusaidia vikundi vipya vinavyoanzishwa, vyama, ushirika wa msingi na ushirika wenye asili ya viwanda unaojumuisha ushirika wa wachimba madini kwa kutoa ushauri wa kina, msaada wa kiutendaji na mafunzo yanayofaa kwa shughuli inayohusika.

## 4.7 Mikakati kwa Aina Nyingine za Ushirika

Ingawa huduma zitatolewa kwa aina zote za vyama vya ushirika, mkazo utaelekezwa kwa ushirika wa mauzo ya mazao ya kilimo, ushirika wa mifugo na taasisi za huduma za fedha ambazo kwa juhudi madhubuti na ushirikiano wa taasisi husika, matunda yanaweza kupatikana katika kipindi cha kati.

## 5.0 USIMAMIZI NA UHAKIKI WA SERA

Sera hii, kama ilivyo ada kwa sera nyingine, imetolewa kwa kuzingatia mazingira yaliyopo ya kijamii na uchumi. Kwa msingi huu, Serikali itafanya tathmini ya mara kwa mara kuona athari ya sera kama msingi wa kuhakiki sera hiyo.

## 6.0 HITIMISHO

Umuhimu wa vyama vya ushirika, kama taasisi za wananchi wenyewe, unaakisiwa katika fursa vinavyotoa katika uhamasishaji wa rasilamali kwa ajili ya maendeleo yao wenyewe. Katika maelezo yaliyotolewa kwa serikali imeonyesha kwa kifupi msaada utakaotolewa kwa ushirika ili utambue nafasi yake katika kuchangia maendeleo ya nchi. Kwa kutumia ushirika, wananchi wanahimizwa kushiriki katika ujenzi wa uchumi wa taifa kulingana na matakwa yao Kwa maana hii, ushirika siyo tu njia ya kupata mafanikio kiuchumi, bali ni chombo ambacho wanachama watakuwa na sauti juu ya sera na mikakati ya utekelezaji wake. Serikali inaamini na kutumaini kuwa wananchi wataitikia wito huu wa kujiunga n taasisi hizi za kidemokrasia.

Sera hii inadhihirisha kuwa serikali inatambua ushiril kuwa ni taasisi za huduma kwa wanachama, tofau kabisa na mifumo mingine ya biashara za binafsi ubia ambao mwelekeo wake ni kupata faida.

Serikali itajitahidi kubuni mikakati inayotekelezeka ili kupata ufumbuzi wa matatizo yanayovikabili vyama vya ushirika wakati huu katika ngazi mbalimbali, yanayotarajiwa na yale ambayo hayajashughulikiwa na sera hii au sera nyingine yoyote nchini.